International Journal of
**Linguistics**
*(IJL)*

# Taswira ya Jamii ya Kisasa kwa Mujibu wa Riwaya Teule za Kisasa za Mwandishi K.W. Wamitila

Janice M. Mutua



International Journal of Linguistics
ISSN 2710-4788 (online)
Vol.3, Issue 1. No.1. pp 1 - 20, 2022

www.iprjb.org

# Taswira ya Jamii ya Kisasa kwa Mujibu wa Riwaya Teule za Kisasa za Mwandishi K.W. Wamitila

[1*] Janice M. Mutua
Mwanafunzi wa Shule ya Mafuzu: Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu
Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
*Mawasiliano: janniec.mwavu@gmail.com
janicemwiks@outlook.com
mutua3000416@student.egerton.ac.ke

**Ikisiri**

**Lengo:** Makala hii inakusudia kuangazia taswira kamili ya jamii ya kisasa kama ilivyodhihirika katika riwaya mpya teule za *Musaleo!* na *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* zilizoandikwa na K.W. Wamitila. Mwandishi amefanikiwa kuieleza jamii ya kisasa kupitia kwa usimulizi wenye simulizi nyingi fupi fupi ambayo ni kipengee kimojawapo cha mbinu ya utunzi ya kimajaribio.

**Mbinu ya utafiti**: Mtafiti aliafikia lengo la utafiti kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo mkabala wa ufasili. Mtafiti ameangazia maandiko yenye uhusiano na jinsi riwaya mpya ilivyoichorea hadhira taswira ya jamii husika. Kipengee cha kimajaribio kilichotumika ni matumizi ya simulizi fupi fupi zilizomo katika simulizi kuu. Data ya utafiti ilikusanywa maktabani kutoka katika uchambuzi wa maudhui katika riwaya za *Musaleo!* (ML) na *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* (MMM). Nadharia ya Usasaleo kama ilivyoasisiwa na Jean Baudrillard iliuongoza utafiti katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

**Matokeo:** Utafiti umebaini kwamba ukosefu wa utaratibu katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali uandishi ukiwemo, waweza kuonekana usiofaa lakini hiyo ndiyo taswira kamili ya maisha katika jamii ya kisasa; hayana utaratibu mahususi. Hali ya mparaganyiko imechukua nafasi kubwa ya maisha ya kisasa. Makala imebainisha kuwa jamii inakabiliana na changamoto nyingi. Aidha imeonyesha jinsi jamii yenyewe inavyojimudu kuzitatua.

**Mchango wa Kipekee kwa Mujibu wa Nadharia:** Mintarafu ya nadharia, mwandishi bunifu ana uhuru wa kuandika jinsi apendavyo, hailazimu kwamba riwaya zifuate utaratibu mahususi. Hii ni kwa sababu maisha katika jamii ya kisasa hayana utaratibu wowote.

**Istilahi Muhimu:** *taswira ya kisasa, jamii ya kisasa, usasaleo, riwaya mpya.*

## 1.0 UTANGULIZI

Jamii ya kisasa aidha inafahamika kama jamii ya mpya. Inawakilishwa na binadamu pamoja na shughuli zake nyingi ziwe za kisiasa, kijamii, au kibiashara kama zinavyodhihirika katika Karne ya Ishirini na Moja. Mabadiliko ya kiubunifu yaliyoshuhudiwa katika uandishi bunifu wa riwaya ya kisasa ya Kiswahili yanawiana na taswira kamili ya jamii ya kisasa (Mutua, 2019). Hivi ni kusema kwamba miundo na mitindo tofauti ya utunzi iliyotumika katika riwaya mpya inashahibiana na jinsi jamii ya sasa ilivyo. Mtunzi wa riwaya mpya zilizochunguzwa K.W. Wamitila kama mwanajamii ametumia mbinu mpya za utunzi kuibua sura kamili ya jamii yake. Hivi leo jamii inapendelea kufanya mambo pasi na kufuata utaratibu maalum. Riwaya iliyochunguzwa imethibitisha kuwa mtunzi wa riwaya za kisasa si mtunzi tu bali ni mwanajamii mwenye uwezo na mwito wa kipekee wa kuimulika jamii na kuiwasilisha kwa msomaji jinsi ilivyo. Katika utafiti huu istilahi riwaya za kisasa, riwaya za kimajaribio na riwaya mpya ya Kiswahili zina maana sawa.

## 2.0 SWALA LA UTAFITI

Jamii ya kisasa imekumbwa na maswala mengi ambayo hayawezi kuwasilishwa kwa kutumia muundo na mtindo mmoja wa kiubunifu hasa katika kazi za fasihi. Waandishi wa kisasa akiwemo K.W. Wamitila wanatumia mitindo mipya ya utunzi katika kuzungumzia maswala mbali mbali yanayoikumba jamii ya sasa kwa njia iliyokiuka uhalisia wa ubunifu uliozoeleka. Hivyo basi utafiti huu umeziba pengo la kitaaluma lilioachwa kuhusu kuwepo kwa mbinu za kimajaribio na uamilifu wake katika uchoraji wa taswira ya jamii ya kisasa kupitia uwasilishaji wa maudhui katika riwaya mpya.

## 3.0 MAPITIO YA MAANDISHI; HISTORIA FUPI YA UANDISHI BUNIFU WA KISASA

Barth (1984) anasema kwamba kitovu cha uandishi wa kimajaribio ni mabara Uropa na Marekani ambapo uandishi wa kimajaribio ulihusishwa na enzi za usasaleo na uzinduzi wa kitaaluma. Katika kitabu chake *Introduction to Literature of Exhaustion* Barth anaeleza kwamba uandishi wa kimajaribio ulipata umaarufu mkubwa katika miaka ya 1910. Waandishi wa kwanza wa kimajaribio ambao walikuwa ni Wazungu na Wamarekani walianza kwa kujaribu hali chache za uandishi wa kimajaribio.

Martha (2008) ametafiti kuhusu riwaya za kimajaribio kati ya miaka ya 1970 – 1980. Kwa mujibu wa utafiti wake riwaya za nyakati hizo zilikuwa na sifa za kimajaribio zilizokuwa changamano zaidi. Akirejelea riwaya *If on a Winter's Night a Traveller* ya Italo Calvino anasema kuwa riwaya yenyewe ilikuwa changamano katika mpangilio wa sura. Baadaye katika mwaka 2005 uandishi wa kimajaribio ulipata mashiko (Barth, 1984). Riwaya zilizobobea katika kipindi hicho ni pamoja na *Pedro Paramo* ya Juan Rulfo wa Mexico, *One Hundred Years of Solitude* ya Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, *The War of the End of the World* ya Mario Vargas wa Peru, *Yo-Yo Boing* ya Giannina Braschi wa Puerto Rico na *Paradise* ya Lezanna Lima wa Cuba, Marekani Kusini. Kinyume na utafiti wa Martha, utafiti huu imechanganua uwepo wa uchangamano kama dhana inayoibainisha jamii ya kisasa.

Kneppert (2016) anaendeleza hoja hii kwa kudai kuwa kipindi cha historia cha *Avant-garde* pia kilitoa mchango mkubwa katika maendeleo na ukuaji wa riwaya za kimajaribio katika Karne ya Ishirini. Waandishi katika kipindi hiki walikuwa na sababu mbali mbali za kutumia mbinu za kimajaribio katika uandishi wa bunilizi walizotunga. Uandishi wa kimajaribio ulichochewa na hali za kisiasa zilizokuwepo wakati huo. Wanajamii walitaka uhuru, haki na usawa katika nyanja zote za jamii zao, uandishi ukiwemo. Walitumia uandishi wa kimajaribio kufahamishana jinsi ya kujinasua kutoka kwa ukoloni. Katika misingi hii utafiti huu umefaniki kutambua kwamba japo jamii ya kisasa inakumbwa na changamoto nyingi, suluhu ni jamii yenyewe. Hivi sasa riwaya imeendelea kukua na kuibuka na mabadiliko mengi kutegemea matukio yanayoshuhudiwa.

Katika Karne ya Ishirini na Moja riwaya za kimajribio zimehusiana na kuibuka kwa matumizi ya tarakilishi na teknolojia za kidijitali. Elliot (2017) katika ufafanuzi wa riwaya *Z213:Exit* ya Dimitris Lyacos anafafanua kuwa ni hadithi iliyoandikwa kwa kurejelea simulizi nyingi fupi fupi. Riwaya ya Dimitris ni hadithi nzuri lakini uchangamano wa mtindo na msuko wake huweza kumchosha msomaji (Elliot, 2017). Kwa misingi hii utafiti huu ulizingatia jinsi mwandishi wa kisasa anavyopanga na kutumia kipengele cha bunilizi nyingi fupi fupi katika riwaya kuu katika uchoraji wa taswira kamili ya jamii ya kisasa. Aidha, mtafiti amejadili athari za tendo la uchupaji wa simulizi fupi fupi katika simulizi kuu na jinsi unavyoakisi jamii ya Karne ya Ishirini na Moja.

### 3.1 Nadharia ya Usasaleo

Baudrillard (1988) anashikilia kwamba riwaya ya kisasa inapaswa kumulika jamii jinsi ilivyo, bila kufuata utaratibu maalum kwa kuwa jamii imejaa fantasia za namna mbali mbali. Hivyo, tanzu za fasihi hasa riwaya zafaa kuwa na simulizi ndogo ndogo ndani yake badala ya hadithi moja ndefu iliyoandikwa kwa njia ya uhalisia kwa sababu jamii ya sasa yenyewe ambayo ndiyo inayoangaziwa na riwaya husika haina utaratibu wa kihalisia. Mtazamo huu uliuelekeza utafiti katika uchambuzi na uchanganuzi wa simulizi ndogo ndogo zinazorejelea maswala na matini tofauti tofauti zilizotumika katika riwaya teule na jinsi simulizi hizo zilivyotumika kubainisha taswira kamili ya jamii ya sasa. Kwa mujibu wa nadharia, maana, maadili na ukweli hupatikana bila kuegemea mbinu au upande mmoja kwa sababu chanzo chake haswa ni jamii. Mhimili huu ulitoa mwanga kwamba fasihi yoyote iwe ya kijadi au ya kimajaribio ni kioo cha jamii. Huitoa taswira kamili ya jinsi jamii ilivyo. Aidha, utafiti uliafikia utambuzi na ufafanuzi wa taswira mbali mbali zilizojificha katika vipande vingi vya hadithi vilivyomo katika riwaya teule. Isitoshe, Utafiti umebainisha majanga yanayozikumba nchi husika na kufafanua jinsi jamii inavyopambana na hali hizo katika juhudi za kujipatia suluhu. Mjadala huu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya usasaleo ifuatayo katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa deta;

i. Riwaya haiwezi kuwa na mpangilio wa moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho bali inatawaliwa na kuwepo kwa vipande vidogo vidogo vya vihadithi vifupifupi ndani ya usimulizi mkuu. (Lyotard, 1984). Mintarafu ya haya, kuna uchangamano mpana katika ploti na usimulizi kwa jumla kwa sababu usimulizi wa moja kwa moja haufuatwi wala hautoshi. Bunilizi nyingi fupifupi ndani ya bunilizi kuu huudhihirisha ulimwengu kwa njia isiyofuata maagizo ya kijadi, jambo ambalo wasanii wa usasaleo wanalitaja kama uhalisia wa kweli. Utafiti huu uliongozwa na mhimili huu kuonyesha na kujadili aina mbalimbali za vipande vya hadithi vilivyomo katika riwaya teule na jinsi mwandishi

anavyovitumia katika uwasilishaji wa ujumbe na uchoraji wa taswira ya jamii ya leo katika riwaya zake za kisasa;

ii. Maana, maadili na ukweli hupatikana bila kuegemea mbinu au upande mmoja kwa sababu chanzo chake haswa ni jamii. Mhimili huu ulitoa mwanga kwamba fasihi yoyote iwe ya kijadi au ya kimajaribio ni kioo cha jamii. Huitoa taswira kamili ya jinsi jamii ilivyo. Haya yaliibuka baada ya uchanganuzi wa kina kuhusu mbinu mbalimbali za kiuandishi za kimajaribio kama zilivyotumiwa katika riwaya teule. Maelezo yametolewa kuhusu jinsi mwandishi Wamitila alivyofanikiwa katika kuwasilisha ujumbe wake akijikita katika mbinu za kimajaribio. Aidha, mhimili huu uliongoza shughuli nzima ya utambuzi na ufafanuzi wa maana mbalimbali zilizojificha katika vipande vingi vya hadithi vilivyomo katika riwaya teule za Wamitila; na

iii. Kitambulisho cha utamaduni wa jamii huundwa kwa nguvu za lugha kwani lugha hiyo hutambulisha jinsi jamii inavyowaza. Riwaya mpya zimetumia tamathali nyingi za lugha katika utunzi wake. Baadhi ya tamathali zilizotumika ni kama vile methali, tashbihi, tashihisi na semi. Ndanimwe mmejificha mambo muhimu ya kijamii. Kwa mujibu wa mhimili huu utafiti huu ulichanganua jinsi tamathali za semi na lugha kwa jumla zilivyotumika kama kitambulisho kamili cha jamii ya sasa.

## 4.0 TASWIRA YA JAMII YA KISASA

Jamii ya kisasa imekumbwa na changamoto na matatizo mengi kama vile magonjwa, vita vya kijamii, vita vya jamii, mizozo ya kisiasa, umaskini na mengineyo (Wacharo, 2013). Aidha athari za utandaazi na teknolojia ya kisasa imechangia pakubwa katika kubaini umbo la la jamii. Katika mataifa yaliyoendelea, mambo mengi na majukumu mengi ya kitaifa hutekelezwa kwa kutumia teknolojia mpya kama tarakilishi, intaneti n ahata mitandao ya kijamii. Kuzuka kwa mbinu mpya za mawasiliano kama matumizi ya rununu, runinga na redio pia ni mambo mapya yanayoieleza jamii ya kisasa. Kwa sababu ya kuwepo kwa mambo haya yote, uandishi bunifu wa riwaya umeathirika pakubwa. Waandishi wa kisasa wanajipata katika hali ambapo lazima wayawasilishe yote yaliyo katika jamii kwa njia ya ubunifu ili wabaini jamii jinsi ilivyo (Mutua, 2022). Hali hii imepelekea kuwepo kwa uandishi wa kimajaribio ambao ni changamano lakini unajitokeza jinsi jamii ya sasa ilivyo. Jinsi jamii ya sasa ilivyojawa na shughuli nyingi ndivyo riwaya za kisasa zilivyojawa na shughuli. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii. Mwamzandi (2013) anafafanua kwamba mambo yaliyo katika jamii ya kisasa hayawezi kuwasilishwa kwa kutumia mtazamo uliozoeleka wa kihalisia pekee.

Kumbukumbu za kihistoria katika riwaya teule zimeonyesha kwamba katika Karne ya Kumi na Tisa nchi za Afrika zilivamiwa na kutawaliwa wa wazungu waliotoka katika nchi mbali mbali za Ulaya (Pakenham, 1992). Wazungu hao waliazimia kuwastaarabisha Waafrika kwa madai kwamba Waafrika waliishi gizani. Taswira hii inawasilishwa katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* msimulizi anaposema kwamba;

> "Akakumbuka hata visa alivyofundisha mwenyewe alipokuwa shuleni: kule **giza** linatamalaki; **wenyeji na wala watu**". **(MMM. UK. 49)**

Giza ni hali ya ukosefu wa mwangaza au nuru. Palipo na giza binadamu hawezi kuona mbele. Katika nukuu hili bara la Afrika linafananishwa na giza. Linaitwa bara lenye "wenyeji wala

watu". Katika enzi za ukoloni nchi za Afrika hazikuwa na maendeleo kama walivyodai wakoloni (Pakenham, 1992). Dhana *giza* imetumika katika simulizi fupi yenye taashira kuikumbusha hadhira sura ya Afrika kabla ya majilio ya wazungu. Wazungu wakoloni walidai kuwa walikuja Afrika ili kuwaondoa wenyeji katika hiyo giza. Msimulizi anaichorea hadhira yake taswira ya Afrika kabla ya utawala wa kikoloni. Hata hivyo, Waafrika wenyewe waliridhika na kufurahia jinsi walivyoishi hata ingawa wazungu waliowaona wakiwa gizani.

Baadaye, Waafrika walipigana na wakapata uhuru kutokana na minyororo ya ukoloni. Hata hivyo, inabainika kuwa bado wanaishi gizani. Baadhi ya mambo yanayoonyesha kuwepo kwa giza katika mataifa ya Afrika ni ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, ufisadi, magonjwa yasiyo tiba, matumizi ya mihadarati na ukosefu wa usalama. Taswira ya jamii ya leo ambayo inaangaziwa ni kuwa, "*wenyeji ni wala watu"*. Hii ni kwa sababu maovu yanayoirudisha Afrika nyuma yanaendelezwa na wenyeji wenyewe. Ufisadi unaoendelezwa na viongozi ni mfano mzuri wa ulaji. Neno "*ulaji"* laweza kurejelea vitendo vinavyosababisha dhuluma, maumivu na machungu kwa raia. Kwa sababu hii wananchi hawawezi kuona mbele wala kuubashiri mustakabali wao wala wa nchi zao.

Nchi ya Kenya ambamo mwandishi wa kisasa anaandikia ilinyakua uhuru mnamo mwaka wa 1963 (Waller, 2014). Baada ya kuanza kujitawala ilikuwa ni jukumu la Wakenya wenyewe kupitia kwa viongozi wao wapya kuboresha hali zao za maisha. Baadhi ya matatizo waliyokabiliana nayo ni magojwa, umasikini na ukosefu wa kusoma na kuandika. Hata hivyo, chini ya uongozi mpya ulioshika hatamu wakati huo, viongozi waliweka ahadi ya kuboresha hali ya maisha ya Wakenya. Je, ahadi zilitimizwa hazikutimizwa? Simulizi ifuatayo inaonyesha taswira ya kiongozi mpya pamoja na majukumu yake.

> "Awaongoze kuhakikisha kuwa *kimbunga cha ufukara* kinachopiga *hakiupukuti majani mti wa ustawi wa jamii yao*. Awaongoze kuhakikisha kuwa hayo maarifa mapya aliyoyapata yamesambazwa kijijini. La nchi nzima. La Bara zima. Si ana ujuzi wa kutosha? Si anazijua siri na jadi yao? Si anaujua ujanja wa rafiki yake aliyeondoka?" **(MMM. UK. 51)**

Kiongozi mpya ana kazi ya kuhakikisha kuwa umasikini umeondolewa nchini. Taashira *"kimbunga cha ufukara"* imetumika katika simulizi hii kurejelea umasikini uliokithiri. Kimbunga ni upepo mkali unaovuma kwa nguvu na kusambaa haraka. Wakati mwingine nguvu zake huharibu mali na kuhatarisha maisha ya binadamu. Isitoshe, *"hakiupukuti majani mti wa ustawi wa jamii yao"*. Giza linapoendelea kutamalaki katika nchi, kuna hatari ya kuwepo kwa umasikini mkubwa ambao huwakumba wengi. Hali hii huwakosesha wenyeji matumaini ya kuendelea kuishi. Kwa jumla kupitia riwaya zinaitaka hadhira lengwa ifahamu kuwa umasikini ni kikwazo kikubwa cha ustawi wa jamii. Hata hivyo, imependekezwa kuwa suluhu la kuondoa giza hupatikana miongoni mwa wananchi au wanajamii wenyewe. Jamii inafahamu kwamba giza ina mwisho, haiwezi kudumu milele. Wenye ujasiri wanaweza kukabiliana na giza yoyote ile. Tumaini la jamii limo katika kizazi kipya ambacho kimeamua kuchukua nafasi yake katika kulisafisha taifa.

> Sasa vuka mto huu wewe na kijana. Mimi sasa siwezi, anayeweza ni Mamanchi na Kijana. Ng'ambo ya pili kuna njia inayopita karibu na mapango. Sehemu yenyewe in

> giza lakini usiogope. Hakuna giza lisilochewa. **(ML. UK. 128)**

Atakayeliondoa taifa na jamii ya sasa kutoka kwenye kilindi cha usumbufu ni mwanajamii mwenyewe. Japo kutakuwa na vikwazo vingi, bidi na ujasiri vitamwezesha kuleta tumaini jipya na tabasamu. Kwa kusema, *"hakuna giza lisilochewa"*, mwandishi anadhihirisha kwamba hakuna tatizo lisilokuwa na mwisho. Dhuluma, madhila na shida zote katika jamii ya sasa ni nyingi na zinaumiza hisia, nafsi na mioyo lakini zina mwisho. Kwa maneno haya mwandishi anaipa jamii ya sasa tumaini la kupata maisha mazri mradi iwe na ujasiri wa kukabiliana na hali zinazoidhulumu kwa lengo la kupata suluhu la kudumu. Zaidi ya haya, ni dhahiri kwamba kuna ng'ambo ya pili iliyojawa na furaha ambayo kila mwanajamii anafaa kuitazamia.

Aidha, ni dhahiri kwamba giza huogofya. Penye giza watu hawawezi kutembea wakiwa huru. Watembeao gizani hutumia kurunzi ili kuleta mwangaza wa kuwasaidia kuendelea na safari. Wanajamii wameacha kutegemea mataifa mengine kwa minajili ya kuondoa giza katika maisha yao ya kila siku. Japo mwanajamii wa sasa anapitia katika hali ngumu inayomzuia kubashiri mustakabali wake, anakazana kwa kushikilia ukweli anaoujua ili afaulu maishani. Ukweli huo ndio mwangaza ambao ni ishara ya tumaini. Vilevile mwangaza ni ishara kwamba japo mambo yamekuwa mabaya sana (kama giza) tena kwa muda mrefu, kuna matumaini ya msaada, fanaka na furaha baada ya kipindi hicho kirefu cha mateso.

Ni kweli kuwa mwanzoni giza linapotanda maishani hapaonekani tumaini lolote lakini katikati ya giza hilo, mna suluhu. Hata hivyo, ifahamike kwamba zoezi la kutafuta tumaini maishani ni jambo linalohitaji juhudi kubwa kutoka kwa wahusika yaani wanajamii wenyewe. Wakati mwingine, kadri binadamu anavyojikaza kukabiliana na giza, hali huendelea kudhoofika na kuwa mbaya zaidi. La muhimu ni uvumilivu na kusonga mbele. Katika riwaya ya *Musaleo!* msimulizi anasema;

> Ilivyoelekea kadiri nilivyojikaza ndivyo nilivyozama katika kiini cha lile giza. …lile giza lilipunguapungua ikawa naweza kuona japo kwa shida. **(ML. UK. 52)**

Giza la matatizo linapozama zaidi, waja huamua kutokata tamaa. Imebainika kuwa kunazo hatua mbalimbali za kujiondoa gizani. Hatua ya kwanza ni kutambua tatizo au aina ya giza inayomkumba mtu. Pili, mtu kufahamu kwamba suluhu yake i mikononi mwake. Hatua ya mwisho ni kusonga mbele na kutokata tamaa hata wakati ambapo mwanga hujaangaza vizuri. Wanajamii wanapofuata Imani hii matatizo hupungua. Msimulizi anasema, *"….giza lilipunguapungua ikawa naweza kuona japo kwa shida*" kumaanisha kuwa hali ya kutoona alikokuwa akielekea ilikuwapo lakini alichagua kuvumilia na hatimaye kufaulu kuitimiza ndoto yake. Hivyo, kizazi cha leo kinaamini kuwa penye nia pana njia. Licha ya ugumu iliopo katika jamii, siri ya kufaulu ni kutokata tamaa na kutia bidii kama inavyobainika katika maneno ya mhusika Musaleo katika riwaya ya *Musaleo!*

> Nilishindwa kuyafungua lakini sikutaka kuishi katika giza. Nilijitahidi kuyafungua **(ML. UK. 130)**.

Ni dhahiri kwamba juhudi za mwanadamu zina uwezo wa kumtoa katika giza lolote linalomkabili. Riwaya za kisasa zinatoa picha ya mwanajamii anayetembea katika ulimwengu wenye dhiki nyingi huku akihakikisha kuwa ameyafungua masikio yake ili asikie mambo muhimu yatakayomfaa katika safari yake ya kutafuta ukombozi. Mahali ambapo anatembelea

pamepewa jina la *"ng'ambo ya pili"*. Mwandishi anasema kuwa ni karibu na mapango na sehemu yenyewe ina giza ila asiwe na hofu. Mwanajamii anapoendelea na safari, jua la tumaini huwaka na kumfanya ajihisi kuwa mwenye nguvu mpya. Anakusanya nguvu zake zote na kuanza kukimbia. Mara kwa mara huanguka kwa kishindo akajaribu kuinuka akashindwa. Wakati mwingine macho hufungika akashindwa kuyafungua. Kwa sababu hataki kuishi katika matatizo haya milele hujitahidi kuyafungua macho yake na kuendelea na safari. Katika jamii ya sasa hakuna shida ambayo inadumu milele. Mwangaza wa furaha na tumaini hupatikana panapo bidii zisizotamauka. Riwaya imethibisha kwa kusema;

> "Nilisema! Nilisema! Nilisema! Ung'amuzi haufi! Giza halitandi milele." Nilimsogea Mamanchi kumuuliza, Je, alikufa lini huyu?" nilisema kwa sauti ya chini lakini aliyasikia. "Minong'ono hainiwezi. Mimi sijafa, bado ninaishi milele! Mimi Veritas sio mtu wa kufa. Nifeje? Uliyekufa ni wewe!" **(ML. UK. 69)**

Simulizi hii inarejelea dhana mbili muhimu, kifo na giza. Kifo ni tukio la kuondokewa na uzima au uhai. Kifo huleta athari hasi katika jamii inayohusika. Ni njia moja ya kusababisha giza lisilokuwa na mwisho kwa mhusika. Katika upande mwingine hali ya kutokufa ambayo imefananishwa na *Veritas* imetajwa katika kipande kifupi cha urejeleomatini. Katika mitholojia ya Kirumi, *Veritas* ni mungu wa kike anayewakilisha ukweli. Msimulizi anasisitiza kwamba ufahamu anaourejelea kama ung'amuzi hauwezi kufa, unadumu milele. Jamii hutumia mmoja wao kuubeba na kuutendesha kazi ung'amuzi. Anayekiriwa jukumu hili hatishwi hata na minong'ono au malalamishi ya wengine. Iwapo kiongozi teule atatoweka kwa sababu yoyote ile, jamii ina Imani kuwa mtu anaweza kufa lakini ukweli utabakia milele. Ukweli ndiyo silaha ya kuwakomboa waja na kuwaweka huru. Katika jamii ya sasa ufahamu kuhusu ukweli unadumu milele. Ukweli ndiyo njia ya pekee ya kuwarudishia waja tumaini lililodidimizwa na dhuluma za viongozi pamoja na hali ngumu za maisha. Jamii ya sasa imeusaka kwa minajili ya kujipatia maisha mazuri kwani ukweli huo ni kifaa cha kuiweka jamii huru.

> Akaufungua na kuangalia nyuma kisha, kama mwigizaji wa filamu, filamu inapokaribia mwisho, akaanza kutembea na kumwonyesha Rama Payo mgongo wake. Akajihisi kama hadhira iliyokuwa ikimwangalia mwigizaji wake akipotelea upande wa pili. Payo akakumbuka wimbi kubwa lililokuwa linaanza kuumuka nchini. Hatimaye punda naye ameelekea kuchoshwa na masogi ya miaka. Aliangalia mbele huko na kuona giza totoro. Akajiwa na taswira ya mti mkubwa uliokatwa na kuanguka chini kwa kishindo. Ile methali ya Kiswahili ya mti mkuu ukigwa, ndege wa mashakani ikamjia. Kisha akasikia sauti za watu wengi waliokuwa wanalia. Wengine wanacheka. Akashangaa hicho kilio cha kicheko kilikuwa na maana gani? **(MMM. UK. 148)**

Giza linalorejelewa hapa linaendelezwa na viongozi dhidi ya wananchi. Riwaya inawachorea wasomaji taswira ya wanajamii ambao wamechoshwa na masogi ya usumbufu waliyoyabeba miaka na mikaka. Istilahi "masogi" ni taashira ambayo imetumiwa kuashiria mateso na madhila wanayoyapata wanajamii kutoka kwa wenye mamlaka ambao wanaongozwa na tamaa. Kwa kuwa ni wanadamu pekee walio na suluhu ya matatizo yanayozikumba jamii zao panahitajika kufanywa uamuzi wa kuandaa mageuzi yenye lengo la ukombozi. Mageuzi yanaamuliwa lakini unapofika wakati wenyewe wanajamii wanakosa motisha ya kuendelea kwa sababu ya kukosa kiongozi mwafaka. Wanajamii wakitazama mustakabali wao wanaona giza totoro, yaani hamna

tumaini lolote la kufanikiwa. Methali, "**mti mkuu ukigwa, ndege wa mashakani"** kuashiria kwamba ukosefu wa viongozi wanaowajibika umeifanya jamii kukumbwa na shida kubwa ya mtu wa kuielekeza. Tegemeo la jamii ni kuelekezwa vizuri. Haya yanapokosekana katika jamii yoyote mlango wa mahangaiko hufunguliwa na kuathiri jamii vibaya. Kwa sababu hii wanajamii hawana uhakika kwamba wakianza watafaulu. Hii ni kwa sababu ya kuwepo kwa giza ya jana inayozidi kuenea;

> Wakati huu giza lilienea kila mahali na sikuweza kujua kama lilikuwa giza la jana au la leo. Nilisimama na kujaribu kuyakodoa macho yangu ambayo sasa hivi yalikuwa yamelizoea giza hilo. Baada ya muda niliisikia ile sauti tena. Mara hii niliweza kuyanasa maneno yake yote. "Alikuwa ni mtu wa matumaini alipokuwa kijana. Kila mtu alimwamini; sote ..e.e.e tulimwamini! Unasikia bwana, soo-ote kila mahali. Kijijini, mijini, nchi nzima, bara zima. Unasikia tena, bara zima! … "Kila mtu aliikumbuka dhiki ya jana. Visa vya kufungwa kwa wenyeji kwenye kongwa na kusafirishwa kwenye meli kama AMISTAD vilikumbukwa na kila mmoja. Dhiki ya kuwa manamba kwenye mashamba ya mikonge ya Wazungu, kufia migondini kurithisha Wareno, watu kuliwa na simba wakijenga reli na umma kucharazwa *djambok*. Vyote vilikumbukwa na kila mmoja. Nakumbuka jinsi kila mmoja alivyotokwa na machozi kisa cha Mamanchi kiliposimuliwa… kule kuna… ashakum: hayasemeki mengine yahe!" **(ML. UK. 91-92)**

Osagie (2000) anaeleza kuwa mnamo mwezi Agosti mwaka 1839 meli ya Kihispania kwa jina *La Amistad* ilitua katika ufuo wa bahari wa kisiwa cha Long jijini New York, Marekani. Shehena yake ilikuwa watumwa, Waafrika hamsini na wanne kutoka katika jamii ya Mende ya Sierra Leone ya sasa. Walikuwa wanaume arobaini na tisa na watoto wanne wasichana wakiwa watatu na mvulana mmoja. Walikuwa wamenunuliwa na Pedro Montes na mwenzake Jose Ruiz ili wakatumike katika mashamba yao ya mikonge kule Cuba (Jones, 1987). Wakati huo Cuba ilikuwa chini ya ukoloni wa Uhispania. Safari ilipokuwa ikiendelea baharini, wale watumwa waliasi, wakawanasa na kuwaua wafanyikazi melini akiwemo mpishi na nahodha kisha wakafanikiwa kuchukua usukani wa meli hiyo. Waliwaamrisha Montes na Ruiz kuirudisha meli Afrika. Hata hivyo, walihadaiwa na meli ikapelekwa hadi Montauk Point, Kisiwa cha Long, Marekani katika safari iliyochukua siku sitini na tatu. Wakati huo biashara ya watumwa ilikuwa imeharamishwa na kupigwa marufuku na mataifa ya Marekani na Uingereza (Jones, 1987). Kwa sababu hii, ingawa wale Waafrika walishikwa na kufungiwa korokoroni, kesi iliyohusiana na uvunjaji wa sheria za kiutumwa ilianzishwa. Waafrika walipata watetezi mahakamani na wakashinda kesi hiyo. Waliruhusiwa kurudi kwao Sierra Leone.

Katika simulizi fupi iliyoboreshwa na matini ya kihistoria, macho ya mhusika Musaleo yanasemwa kuwa yalikuwa yameizoea giza. Hakuwa na uwezo wa kuona mbele katika safari yake. Safari hii inalinganishwa na ile ya watumwa waliokuwa katika meli ya *La Amistad*. Hawakuwa na matumaini yoyote ya kupata uhuru wao. Hawakuwa na uwezo wa kubashiri jinsi maisha yao ya baadaye yangekuwa. Katikati yao pakaibuka kiongozi ambaye alikuwa chemichemi ya tumaini kwa watumwa wengine. Kiongozi huyu analinganishwa na Musaleo ambaye aligeuka kuwa kipenzi cha wengi. Riwaya zimesema kuwa watu wote mahali popote wapatikanapo pawe kijijini au mjini walimfahamu kama mtu mwenye matumaini. Wote waliomfahamu walimwamini. Historia ya maisha ya hapo awali ya utumwa ambayo yalikuwa

machungu yaliyojaa dhiki yanatolewa katika simulizi hii kama kumbukumbu. Hadhira inakumbushwa jinsi Waafrika walivyosafirishwa katika meli huku wakiwa wamefungwa kwenye kongwa ili wasitoroke.

Mkombozi wa mwafrika ni mwafrika mwenyewe. Mwafrika aliyeikata minyororo ya utumwa katika *La Amistad* alithibitisha kuwa hakuwa binafsi kwa kuwasaidia wenzake kujifungua. Baada ya kuwaweka wenzake huru, kwa pamoja waliungana kuusaka uhuru kikamilifu. Simulizi ya *La Amistad* inaonya jamii dhidi ya ubinafsi. Ubinafsi ni ugonjwa wenye uwezo wa kuliangamiza taifa. Kwa upande mwingine, umoja ndio silaha ya ufanisi wa taifa. Kinaya ni kwamba jamii ya sasa ina mbinu zote zinazohitajika katika kujitwalia ukombozi lakini haizitumii.

Watumwa walipata dhiki ya kutumikishwa katika mashamba makubwa ya mikonge. Wengine walifia migodini mikononi mwa mabwana zao, Wareno. Waliosalia walipata dhiki ya kuliwa na simba wakijenga reli huku wananchi wengine wa kawaida wakiumizwa kwa kucharazwa mijeledi. Kulingana miktadha ambamo simulizi hizi zimetumiwa riwayani msimulizi ameiwasilisha jamii ambayo bado i katika ukoloni na hali kadhalika ukoloni mkongwe ambao bado unadhihirika katika jamii ya sasa. La muhimu zaidi ni ufahamu kwamba binadamu wa sasa ndiye aliye na uwezo wa kujikomboa kutokana na dhiki inayompata. Hata hivyo, inahuzunisha kwamba wanajamii wamesahau historia yao, hali inayomfanya mwandishi wa riwaya mpya kuiwasilisha historia hiyo katika riwaya ili waisome. Wanajamii wana jukumu la kusimama imara na kutetea asili yao kama inavyodhihirika katika usemi huu wa mhusika Mzee katika riwaya ya *Musaleo!*;

Nitarudi **kondo yangu** ya nyuma imezikwa huku! **(ML. UK. 4)**

Istilahi "kondo" inayorejelea imani za kijadi inabaini insi jamii inavyothamini kitu chochote ambacho inamiliki. Kondo ni mfuko anaokalia mtoto ndani ya tumbo na ambao hutoka baada ya mtoto kuzaliwa. Ni kiungo muhimu katika ukuaji wa mtoto. Uunganishaji wake na mtoto huonyesha uhusiano usiotenganishika baina ya mtoto na mama ila tu baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Hata hivyo, baada ya mtoto kuzaliwa, uhusiano huo huendelezwa na nguvu za damu na mapenzi. Katika muktadha huu, msimulizi anarejelea umilisi wa ardhi (tafsiri yangu). Riwaya inaeleza kwamba mahali binadamu alipozaliwa pana historia muhimu kuhusu asili na jadi yake. Hivyo, mwanajamii anamiliki ardhi ambamo alizaliwa, yaani pale kondo yake ilipozikwa. Umilisi unaolinganishwa na kondo unatiliwa maanani kiasi kwamba hata binadamu husika akiondoka au akiondolewa anaweza kurudi na kudai ardhi yake kwa ushahidi kwamba kondo yake imezikwa mle. Riwaya mpya zimepanua wazo hili kuhusu matatizo ya umiliki wa ardhi katika mataifa yanayoendelea na kuonyesha kuwa iwapo wanajamii wangeheshimu asili zao za kijadi hakungekuwa na matatizo ya umiliki wa ardhi. Mwanajamii hawezi kutenganishwa na ardhi yake. Yeye ndiye mwenye suluhu ya matatizo ya ardhi imo yanayoshuhudiwa katika jamii. Kinachohitajika ni kufanya uamuzi wa busara kisha kutenda haki kwa mujibu wa sheria zilizowekwa kwani zinatambulika vizuri na wanajamii. Kumbukumbu za yaliyopita ni njia nzuri ya kuwasaidia wanajamii kutafuta suluhu la matatizo yao. Mwanajamii daima hawezi kutenganishwa na ardhi yake.

Kumbukumbu ni ganzi nzuri ya kupoza maumivu. Kufisha ganzi ni kitendo cha huduma ya kwanza cha kupunguza makali ya uchungu baada ya kupata maumivu au kujeruhiwa. Ingawa

binadamu anapitikiwa na mambo mengi yanayomsumbua anaweza kuyasuluhisha kwa kupunguza makali yake kwa kumbukumbu za mazuri yaliyompitikia wakati mmoja katika maisha yake. Hivyo, kumbukumbu ni mbinu moja ya kusuluhisha matatizo. Hali kadhalika katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* kumbukumbu imeangaziwa kama suluhu;

> **Akanyamazisha sauti** za akina Marugurugu na wenzake. Mwenzake naye akamtumia ujumbe wa kuja kuangalia jinsi alivyokuwa amepiga hatua. Ujumbe wa kufuatilia kujua kama msaada wao ulikuwa wa kufaa au la. Ujumbe huu ndio uliomfikishia barua iliyotokea kwao. Akakumbukushwa jambo ambalo alielekea kulisahau. Ilikuwa Barua ya Kumbukumbu. Ahadi ni deni. **(MMM. UK. 75)**

Mkoloni pia ana kumbukizi zinazoliwaza moyo wake. Baada ya kuondoka kwake, aliacha waliobaki waendeleze sera zake kwa kuendeleza ukoloni mkongwe. Walihakikisha kwamba wamefisha nguvu za uwezekano wa mapinduzi ya aina yoyote kwa kudidimiza usemi wa viongozi. Usemi "kunyamazisha sauti" umetumika kueleza vilio vya wanyonge vinavyokosa kusikizwa na "wenye nguvu" yaani viongozi wa enzi hizo za ukoloni mamboleo. Msimulizi anaendelea kusema kwamba vitendo vyote vya wakoloni vilihifadhiwa katika "Barua ya Kumbukumbu." Kama vile inavyowasilishwa riwayani, kumbukumbu ni njia moja ya kuliwaza akili baada ya kipindi kirefu cha kumkosesha mwanadamu amani. Mwanajamii anapotazama nyuma na kuona yote yaliyompitikia na jinsi alivyojikomboa analiwazika. Hata ingawa mkoloni alikuwa ameshaondoka kutoka nchi ambayo kwa wakati mmoja aliitawala, alijiliwaza kwa kumbukizi za awali. Alikumbuka jinsi alivyokuwa na mamlaka juu ya kila hali hata nafsi za wenyeji. Alikumbuka jinsi alivyotawala sekta zote kama vile uchumi, siasa, elimu na maisha ya jamii kwa jumla. Haya yote yalipojumuika akilini pake kama kumbukumbu alifarijika. Baada ya kumbukumbu hizi mkoloni alimotishwa kurudi kwa mara ya pili barani Afrika, wakati huu kwa kutumia ujanja kama inavyoelezwa hapa;

> …Sasa yeye anachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kuwa amefungua njia. Atafute ujanja wowote ule lakini sharti, vyovyote atakavyofanya, afanikishe kupasuliwa kwa huo utumbo wa ardhi na kukakatuliwa kwa majabali hayo ili kufichua yaliyokuwa ndani. …Watu husema unaweza kutoka walipo ndovu ukashusha pumzi kumbe unaelekea waliko mbogo. **(MMM. UK. 75-76)**

Mapito ya wakoloni wa jadi yaliandaliwa na wamisheni. Nia ya wamisheni hao ilikuwa kueneza dini ya Kikristo. Vivyo hivyo, wakoloni wachache waliobaki barani Afrika wengi wao wakiwa wafanya biashara, walimu na wanasiasa walikuwa na jukumu moja muhimu la kuandaa mapito ya wakoloni wakongwe. Haya ndiyo yanayorejelewa katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* kama *"kufungua njia."* Msimulizi anazidi kufafanua kuwa wazungu wakoloni walitumia ujanja ili wapate rasilimali zilizohifadhiwa Afrika kwa ajili ya viwanda vyao kule nyumbani. Katika riwaya msimulizi anasema, *"afanikishe kupasuliwa kwa huo utumbo wa ardhi na kukakatuliwa kwa majabali hayo ili kufichua yaliyokuwa ndani."* Nia kuu ya wakoloni ilikuwa kutambua utajiri wa madini yaliyofichika ardhini, kuyachimba na kuyasafirisha Ughaibuni ili yatumike katika viwanda vyao. Kwa kutwaa rasilimali za Afrika, wakoloni walichangia katika kufifiza uchumi na maendeleo ya Afrika kama anavyosema Rodney (1981), hali ambayo inashuhudiwa hadi sasa. Katika muktadha huu, jamii ya Afrika imedorora kiuchumi.

Jamii ya sasa imekataa katakata kujiingiza katika matatizo yaletwayo na ukoloni mamboleo kwa kuwaaminia wageni rasilimali zake. Aidha, jamii inashikilia kauli kwamba "kikulacho ki nguoni mwako." Jamii ina ufahamu kwamba inafaa kutambua kuwa waangalifu kuhusu mienendo viongozi wa mataifa yao baada ya kupatikana kwa uhuru. Japo mkoloni alikuwa dhalimu, viongozi Waafrika wamekuwa dhalimu zaidi. Riwaya zimebaini kwamba kuwa na kiongozi Mwafrika ni kama, "*kutoka walipo ndovu ukashusha pumzi kumbe unaelekea waliko mbogo".* Usemi huu unamwashiria ndovu kama mnyama mkubwa, mwenye nguvu nyingi na ambaye wakati mwingine huwa mharibifu sana. Kwa upande mwingine mbogo ni mnyama mkali na mharibifu. Akilinganishwa na mbogo, ndovu ni mtulivu. Kwa hivyo ni hatari zaidi kusazwa na ndovu kisha kutupwa au kuelekezwa kwa mbogo. Picha inayojitokeza ni kwamba Afrika hufikiri matatizo yake yalitokana na mkoloni pekee ila kwa mujibu wa riwaya teule adui wa mwafrika ni mwafrika mwenyewe. Mwafrika ndiye aliyejiingiza katika hali ya kifo cha kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kifo ndio mwisho wa uhai (Blum, 2004). Kifo hutokana na sababu aina aina kama vile, umri mkubwa unaosababisha michakato ya kimsingi mwilini kusimama polepole na ajali zinazoharibu viungo muhimu mwilini. Mambo mengine yanayosababisha kifo ni pamoja na ukosefu wa chakula, maji, hewa au kinga dhidi ya mazingira magumu, athari haribifu kutoka kwa viumbe wengine au mazingira (Lunde, 1979). Vilevile, kifo hutokea ikiwa binadamu amekuwa na muda mrefu wa maisha unaoruhusu makosa na kasoro kujumuika na kusababisha madhara kama saratani na magonjwa mbalimbali yanayovuruga michakato ya uhai hadi kuyasimamisha maisha (Gilbert, 2003). Kifo hutamausha zaidi kwa sababu hakuna kinachobaki baada ya mauti (Yuswanto, 2015). Ni mwisho wa binadamu kimwili na kiroho. Kifo kimefananishwa na mgeni mwenye wivu mwingi anayetembea katika nchi ng'eni. Ni mgeni mwenye wivu kwa sababu huchukua kile kilichonawiri na kinachotegemewa na jamii pamoja na taifa. Huu ni ulinganisho tu wa kifo cha kiuchumi na kisiasa katika jamii ya kisasa. Kila hali ya maisha yake imekufa kwa sababu mbali mbali. Mambo hayo ni pamoja na dhuluma, ubinafsi, uzorotaji wa uchumi na uhasama wa kikabila. Maafa haya yote yamesababishwa na uongozi mbaya. Yanatishia kuziangamiza jamii za Kiafrika za kisasa wakati zinapohitajika zaidi. Kifo cha jamii ni kama mtu anayejizungukia huku na kule. Anapoona mlango wowote ulio wazi anajitoma ndani ghafla na kuwanyakua waliomo. Kulingana na riwaya, jamii ya sasa ndiyo inayochangia katika maangamizi yake kwa kufungua milango yake kwa yeyote anayetaka kuingia. Kando na haya riwaya za kisasa zinaitaka jamii iweke mikakati kabambe kuhusu uwekezaji katika mataifa husika bila kuwategemea wageni wasioaminika. Kwao, riwaya zinasema, "

> Mizizi ya mti wa uwezo wangu alikuwa anaanza kuitafuna chini kwa chini kama fuko. Ilibidi niwahi tumba la uovu kabla halijachanua na kutapakaza harufu ya uhasama nchi nzima. Wiki tatu baadaye profesa alikufa katika ajali ya barabarani. Niliongoza nchi nzima katika maombolezi ya kifo hicho. Jamaa zake niliwaahidi kuwasaidia. "Ikiwapata shida yoyote, nipigieni simu tu!" niliwakumbusha. **(ML. UK. 69)**

Katika ulimwengu wa usomi profesa ni binadamu aliyesoma kwa mapana na marefu. Ana ufahamu wa mambo anuwai tena kwa undani. Kwa mujibu wa Nyabunga (2005) profesa anaona yale wengine wasiyoyaona. Profesa anayerejelewa katika nukuu hii alifanya utafiti kuhusu hadithi moja ya kijadi katika jamii yake (kisa cha Mamanchi), mama mmoja aliyedaiwa kuwa

dadake kiongozi wa taifa wakati huo aliyefahamika kwa jina la Mzee. Matokeo ya utafiti huo hayakuufurahisha uongozi wakati huo. Baada ya wiki tatu profesa alifariki katika ajali ya barabarani iliyokuwa tatanishi. Mzee aliliongoza taifa katika maombolezi na mazishi ya profesa. Katika hotuba yake wakati wa mazishi, Mzee alieleza jinsi kifo cha profesa kilivyoacha pengo kubwa ambalo halingezibika. Kama ilivyo kawaida ya viongozi wa kisasa, Mzee aliongeza kuahidi kuisaidia jamaa ya profesa kwa vyovyote vile. Katika jamii ya sasa imebainika kuwa watu werevu ambao wanaona yasiyoonekana na wengine hawatakikani katika jamii. Labda ung'amuzi huu unaeleza jinsi wasomi kama profesa hutoweka katika hali zisizoelezeka kila wanapoonyesha uzoefu wao wa ujuzi. Katika simulizi fupi iliyotumiwa na msimulizi wa riwaya ya *Musaleo!*, taswira tofauti tofauti za jamii ya kisasa zimebainika katika matumizi ya taashira *kuitafuna nchi kama fuko"* na *"tumba la uovu"*. Kwanza, katika jamii ya kisasa viongozi huwahofia watu wenye akili nyingi yaani wasomi kwa sababu wana uwezo wa kuweka hadharani mambo yafanywayo sirini hasa katika ngazi za uongozi. Pili, watu hao wenye ujuzi na wanaotegemewa katika jamii wanapofariki, daima viongozi hao hao huonyesha unafiki wao hadharani kwa kutoa ahadi ambazo hatimaye hutokea kuwa za uongo. Tatu, binadamu mwenye ujuzi katika mataifa yanayoendelea hana haki ya kuishi; uhai wake humtoka kwa njia tatanishi. Kwa hivyo inabainika kuwa profesa hangeishi kwa sababu ya ufahamu wake kuhusu mambo mbali mbali yaliyoikumba jamii yake; kwake kuyasema hadharani kulikuwa kama kujitia kitanzi. Baada ya mazishi ya mhusika ahadi za viongozi hubakia kuwa ahadi tu. Nne, hakuna kiongozi yeyote anayetaka kuambiwa ukweli kuhusu jinsi anavyotekeleza kazi yake hasa pale anapofanya makosa. Matukio yaliyotajwa yanaashiria ukosefu wa uhai katika usomi na maendeleo katika jamii. Hali hii inazidi kufafanuliwa katika simulizi fupi inayomhusu Malkia Diana Frances Spencer wa Uingereza na mpenzi wake Dodi Al Fayed wa Misri. Japo vyao vilikuwa vifo kwa sababu ya tukio la kimapenzi ni dhahiri kwamba kifo ni kifo yaani athari za kifo zina machungu kwa jamaa licha ya kile kilichosababisha kifo chenyewe. Kwa mujibu wa riwaya teule na kwa vyovyote vile, kifo husababisha kupotea kwa matumaini na raha maishani.

Katika jamii ya sasa, simulizi fupi hii imetumia taashira "kifo" kuzidi kubainisha kuwa hakuna siri isiyoweza kuvumbuliwa wala kutambuliwa. Licha ya haya, jamii imekosa maadili hasa kuhusu mahusiano katika ndoa. Msimulizi ametumia simulizi fupi kuhusu hatima ya mapenzi baina ya Malkia Diana Spencer na Dodi Al Fayed kufafanua. Hadithi yenyewe inaonyesha ukweli kwamba mapenzi yanapokatizwa hamu na tamaa ya kuishi hukatizwa pia. Hii ndiyo sababu mapenzi yanafananishwa na kifo. Mapenzi hukatizwa na mambo aina aina lakini adui mkuu wa mapenzi ni kifo. Baada ya kupatana na kuchumbiana, Diana na Dodi pamoja na wazazi wao walikuwa na matumaini ya maisha mazuri ya baadaye lakini hayo yote yalikatizwa na kifo. Mintarafu ya simulizi fupi hii riwaya imewasilisha taswira kwamba kifo kinachotokana na mapenzi hutamausha zaidi. Hata hivyo, mwandishi ameitaja hadithi ya Diana katika usimulizi mkuu pasi na kuisimulia kwa matumaini kwamba hadhira itajaliza mapengo aliyoyaacha na kupata ung'amuzi wa funzo analowasilisha. Ili kupata taswira kamili ya jamii ni sharti hadhira ifahamu muktadha wa simulizi iliyorejelewa kwamba: baada ya Malkia Diana kutamaushwa na mapenzi baina yake na mumewe ambaye ni Mwanamfalme Charles Philip Arthur George Mountbatten kutumbukia nyongo na kupewa talaka, Diana alijipatia mpenzi mwingine, Dodi Al Fayed kutoka Misri (Bradford, 2007). Hata hivyo, tumaini lake jipya la mapenzi lilikatizwa na kifo cha ajali barabarani kilichotokea katika hali tatanishi. Wakati mmoja wapenzi hawa wawili

walialikwa na babake Dodi kujivinjari katika ziara ya majini kule Corsica na Sardinia ndani ya meli ya kibinafsi na kifahari maarufu kama *Jonikal* (Bradford, 2007). Baada ya kufahamu kuhusu uhusiano wa Diana na Dodi wanahabari waliwafuata kila uchao (Junor, 2005). Mnamo tarehe mbili Agosti 1997, mpigapicha tajika Mario Brenna aliwasili Sardinia kwa mwaliko wa Diana (Smith, 2007). Baada ya siku mbili alipiga picha za Dodi na Diana zilizopachikwa jina, "picha za busu" na kuzichapisha (Snell, 2013). Agosti tarehe ishirini na moja Malkia Diana alijiunga na mpenzi wake tena kwa ziara ya pili iliyofanyika Paris, Ufaransa (Bradford, 2007). Habari kuhusu uhusiano wao zilikuwa zimeenea kote ulimwenguni kwa kasi kiasi cha kuwafanya mapaparazi kuwafuata kila mahali. Wanahabari pia walichapisha habari kuwahusu Diana na Dodi kila uchao. Mnamo saa sita tarehe thelathini mwezi Agosti mwaka 1997 wapenzi hawa waliondoka kuelekea Paris (Smith, 2007). Walipotua katika uwanja wa ndege katika mji wa Le Bourget, Paris wanahabari na mapaparazi walikuwa tayari wakiwasubiri ili kuutangaza uhusiano huo kwa dunia nzima. Kwa mujibu wa Brown (2008) Dodi alimwelekeza dereva mjini Bois de Boulogne kinyume na mpango wa awali wa kuelekea Ritz kwa lengo la kuwaepuka wanahabari na mapaparazi. Baadaye walienda hadi kwenye makazi ya kifahari ya Fayed kule Rue Arsne-Houssaye. Kinyume na matarajio yao, mapaparazi walizidi kuwafuata. Katika hali hii gari la Diana na mpenzi wake aina ya *Mercedes Benz* lilianguka na kubingiria kutokana na kuendeshwa kwa mwendo wa kasi (Brown, 2007). Diana na Dodi walipelekwa hospitalini ambamo kifo chao kilithibitishwa (Bradford, 2007).

Kisa cha Diana na Dodi kimetumiwa katika riwaya teule kubaini kuwa kifo cha aina yoyote kina uzito wa kuleta huzuni isiyo kifani katika jamii. Ni onyo kwa jamii ya sasa kwamba ikiazimia kuishi ni sharti ijiepushe na hali zinazoweza kusababisha mauko miongoni mwa wanajamii wake. Jamii ya sasa isiyo na maadili ijapo wakati wa kuonyesha mapenzi na kuchumbiana inahimizwa kuendeleza maadili yanayokubalika. Kwa mara nyingine, riwaya zimesisitiza kwamba jamii ndiyo yenye suluhu la matatizo yanayoikabili. Kauli hii imetiliwa mkazo kwa matumizi ya swali la balagha kwamba; *"…uhai na kifo. Riale kwa ya pili?"* Kwa maneno mengine kile kinachopitishwa riwayani ni kwamba jamii itakuwa jinsi itakavyojichagulia kuwa. Uhai na kifo ni matukio mawili yanayoshabihiana kama shilingi kwa ya pili ambayo yako mikononi mwa jamii yenyewe.

Hoja ya "kifo" kilichokithiri katika jamii ya sasa kinaweza tu kuangamizwa na jamii yenyewe. Suluhu la jamii ni jamii. Ili kubainisha taswira ya jamii ya sasa kuna hadithi (ngano) iliyosikika kanisani wakati wa sherehe ya arusi iliyorejelewa. Hadithi husika ni kifaa muhimu cha kuijuza jamii kwamba ili kupiga hatua kimaendeleo na kuimarisha huduma kwa wanajamii wote ni sharti kila mmoja afishe makosa ya kihistoria na kuyazika katika kaburi la sahau. Maneno katika usimulizi yalisemwa na mhubiri kwa bwana na bibi arusi. Alikuwa akiwapa wosia kwamba iwapo watapenda kuishi vizuri katika maisha ya ndoa itawabidi wafishe "*jana yao*". Jana inaashiria wakati uliopita. Mhubiri alisistiza kuwa ni lazima ya kale miongoni mwao kama ubinafsi yafe ili umoja wao uzaliwe. *"Ni lazima mbegu ife ili mche uote".* Isitoshe, kifo hutangulia mapenzi kama ilivyokuwa katika kisa cha Yesu Masihi. Ilibidi afe msalabani ili wenye dhambi wapokee msamaha kwa mujibu wa dini ya Kikristo. Kwa hivyo, kifo chake kilikuwa chanzo cha mapenzi kwa wenye dhambi. Kwa mujibu wa haya jamii ya kisasa inawajibika katika kufisha historia yake hasi ili maendeleo yapate kuota. Ukosefu wa huduma bora ni mambo yanayozalishwa na ukoloni mamboleo ambao ni zao la historia. Kitendo cha

*"kufisha historia"* ndiko kuzaliwa kwa mara ya pili. Hivyo, taswira ya jamii ya sasa ni kwamba kutakuwa na kizazi kipya au tumaini jipya la jamii. Jamii mpya hiyo itakuwa ile iliyosahau jana yake kwa kufisha hali hasi zilizoikumba na kuzingatia mienendo mipya kwa lengo la kuinufaisha kama wasemavyo wahenga "yaliyopita si ndwele tugange yajayo."

> "Je, unaamini kuzaliwa mara ya pili?" "Kuzaliwa kisha kufa na kuzaliwa tena." **(ML. UK. 78-79)**

Katika riwaya ya *Musaleo!* kuzaliwa, kufa kisha kuzaliwa tena ni tendo la uhalisiajabu yaani jambo lisilowezekana katika uliwengu wa uhalisia. Kipengele hiki cha kimajaribio kimeambatanishwa na taashira ili kuwasilisha maudhui ya ukoloni, ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Katika jamii ya leo, ukoloni ni jambo linalodumu milele. Hii ni kwa sababu hata baada ya Waafrika kujipatia uhuru, bado wanatamani kutawaliwa na kuongozwa na mkoloni waliyemfukuza. Mwafrika daima ameweka tumaini la maendeleo yake katika matendo na mipango ya wageni aghalabu wazungu. Badala ya kukuza uchumi wake, daima anategema misaada kutoka "nje". Kwa mfano, badala ya kuwaamini madaktari wake waliofunzwa na kuhitimu, kila anapokuwa mgonjwa matibabu yafaayo ni ya ughaibuni. Isitoshe, Mwafrika anaamini masomo katika nchi nyingine nje ya Afrika badala ya kuimarisha elimu katika taifa lake. Mambo haya yote yanazidi kumzamisha katika lindi la madeni, jambo linalochangia pakubwa katika kifo cha taifa lake. Riwaya ya *Musaleo!* inaona utegemezi kwa wageni uliokithiri kwa minajili ya ufanisi kama tendo na mbinu ya mkoloni ya kuendeleza ukoloni wake dhidi ya Mwafrika. Jamii ya sasa inaonyesha taswira ya ukosefu wa uwezo wa kujiamulia maswala yake. Katika taifa lolote linaloendelea ni sharti kuwe na mipango mizuri ya kuimarisha elimu, kuwalipa wafanyakazi mishahara mizuri, kuwepo kwa barabara nzuri, kuimarisha hali ya mawasiliano na kuwa na chakula cha kuwatosha raia wote. Kinyume na haya Waafrika wanaamini kuwa fanaka yao itapatikana tu kwa kuzitegemea nchi za nje. Kwa sababu hii wanawekewa vikwazo ambavyo vinawadidimiza zaidi (Nanjira, 2010). Ndio maana riwaya teule zinaimulika hali hiyo na kukiri kwamba ukoloni hauwezi kuisha Afrika. Unazaliwa, unakufa na kuzaliwa tena, yaani unabadilisha majina tu. Ukoloni wa kwanza ulikuja na dhuluma ilhali ukoloni mamboleo unakuja na mambo mawili: dhuluma na vikwazo. Nyabunga (2005) anataja baadhi ya vikwazo vinavyowekewa nchi zinazotawaliwa na kasumba za ukoloni kama, kupunguza idadi ya wafanyakazi, kuanzisha viwanda vinavyofaidi nchi za kigeni pekee ili ziuzwe kama rasilimali viwandani na kununua bidhaa zilizotengenezewa ugenini. Maswala mbali mbali ya siasa pia yanawekewa masharti kama vile kuwa na vyama vingi vya kisiasa na kubinafsisha mashirika ya kiserikali ili kuleta uhuru na demokrasia miongoni mwa raia. Kwa sababu hizi ukoloni mamboleo unajigamba kwamba hauwezi kufa hata iweje kama inavyothibitika tena katika uzungumzi nukuu hili;

> Nilimsogea Mamanchi kumuuliza, Je, alikufa lini huyu?" nilisema kwa sauti ya chini lakini aliyasikia. "Minong'ono hainiwezi. Mimi sijafa, bado ninaishi milele! Mimi Veritas sio mtu wa kufa. Nifeje? Uliyekufa ni wewe!" **(ML. UK. 69)**

Athari za ukoloni barani Afrika zimekithiri kufikia kiwango kwamba wageni wasio wenyeji wanajigamba kwamba Afrika ndiyo itakayokufa wala si wao. Mkoloni hawezi kufa kwa sababu anatawala kila sekta ya maisha ya Mwafrika kama vile uchumi, elimu, siasa na maisha ya jamii kwa jumla. Vilevile, athari za utandaridhi zinatishia kuiangamiza jamii ya Afrika kila uchao

(Nyabunga, 2005). Ukweli huu unabainishwa na usemi ufuatayo unaopatikana katika riwaya ya *Musaleo!*;

> "Nilisema kuwa Ukolongwe hakuzikwa: tazama kaburi lake bado li wazi. Niliwaambia wasiojifunza kutokana na historia wamelaaniwa kuyarudia makosa ya jana: makosa ya historia yenyewe!" **(ML. UK. 70)**

Mtu anapokufa na kuzikwa huanza kusahaulika pole pole. Mazishi huashiria mwisho wake, uwepo wake, kazi zake, na athari zake. Lakabu Ukolongwe imetumiwa kuashiria ukoloni-mkongwe. Jina jingine la ukoloni-mkongwe ni ukoloni mamboleo. Lakabu hii inarejelea jinsi nchi tajiri zilizoendelea huingilia maswala ya nchi zinazoendelea hata baada ya nchi hizo kupigana na kujipatia uhuru (Barongo, 1980). Hata hivyo, tabia hii ni kinyume cha Azimio la Umoja wa Mataifa (Birmingham, 1995). Kwa mujibu wa riyawa ya *Musaleo!* ukoloni wa aina hii unawakilishwa na athari hasi kama inavyobainishwa na Suret-Canale (1988) kwamba wafanya biashara binafsi na makampuni ya biashara za kigeni huendelea kunyonya rasilimali za mataifa yanayoendelea muda mrefu baada ya enzi za ukoloni. Ndio maana riwaya zimesema kwamba mhusika Ukolongwe hakuzikwa na hata kama alizikwa kaburi lake li wazi. Katika riwaya hii simulizi fupi yenye lakabu Ukolongwe inabainisha jinsi athari za ukoloni zingali hai katika mataifa ya Afrika yanayoendelea hata baada ya kujipatia uhuru. Hata hivyo, wembe ni ule ule. Afrika ni lazima isahau "jana" yake ili ipige hatua mbele kimaendeleo. Ni sharti itupitilie mbali historia dhalimu na kukumbatia nguvu na uwezo wake kama taifa huru. Haya yatawezekana ikiwa Waafrika watatambua kuwa wako usingizini na sharti wafahamu kwamba wao wenyewe ndio wenye uwezo wa kujitoa katika usingizi huo.

> "…"Nilimwonya akakataa. Ilikuwa lazima siku moja atafanya jambo la kumuudhi Mzee!" alitulia kisha akaendelea kama mtu anayejisemea, "Nilisema yule ni kizalia cha Ukolongwe wakakataa! Sasa wanayaona haya! Watu wanalala kwa miaka na miaka, usingizi wa aina gani huu?" **(ML. UK. 71)**

Kwa mujibu wa riwaya mpya viongozi katika jamii ya kisasa bado wanaendeleza dhuluma. Wameelezwa kama vizalia vya Ukolongwe. Athari za ukoloni mkongwe ndizo zinazowafanya kuendeleza ukoloni baada ya uhuru hali maarufu kama ukoloni-mamboleo. Kwa mujibu wa riwaya za kisasa athari hizi zinajitokeza katika tabia kama ubinafsi, wizi wa mali ya umma, uchafuzi wa mazingira na unyanyasaji. Wanaoiba mali ya umma wanafanya hivyo kwa kisingizio kwamba kila mtu nchini ni mwizi. Kama ilivyo kwamba suluhu la Mwafrika ni Mwafrika, adui mkubwa wa Mwafrika ni Mwafrika mwenyewe. Jamii ya sasa imejawa na unafiki na uongo. Wanaosema uongo wanajionyesha kama wakweli.

> "…nani asiyeiba nchi hii? Alijiuliza. Nani ambaye anaweza kuaminiwa kwa kusema ukweli? Alishangaa. …anayesema ukweli ni mimi tu, mimi Mzee! **(ML. UK. 2)**

Simulizi fupi hii iliyowasilishwa kwa njia ya uzungumzi nafsia hapa ina sifa ya balagha. Maswali aliyoyauliza mwandishi hayahitaji majibu. Mazungumzo haya yanabainisha kwamba tatizo moja sugu katika nchi za Kiafrika zinazoendelea ni wizi na ubadhirifu wa mali ya umma. Wanaoendeleza wizi ni viongozi ambao mara nyingi wanajitokeza kama waja wasioridhika. Kila wanapoiba mali ya umma wanajiliwaza kwa maneno, *"nani asiyeiba nchi hii?*" kumaanisha

kuwa kila mtu ni mwizi nchini kwa hivyo wizi si kitendo kibaya. Sura ya jamii inayobainika ni kuwa viongozi huwadhulumu raia kwa kupora rasilimali zake na kusingizia kuwa ni sawa kwa sababu kila mtu anaiba. Uporaji wa rasilimali za umma ndio unaosababisha umaskini uliokithiri, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na ukosefu wa huduma bora. Hali ya dhuluma inasababisha uasi dhidi ya serikali. Raia wanajiunga pamoja katika makundi ya ukombozi ili kutafuta suluhu ya matatizo yanayoikumba jamii yao. Serikali nayo hupinga mapinduzi kwa nguvu nyingi. Wakati mwingine vijana hutumiwa na walio mamlakani kupinga mapinduzi labda kwa sababu hawana kazi nyingine. Vijana katika mataifa yanayoendelea wanatumiwa vibaya na viongozi. Ujumbe huo umewasilishwa katika simulizi fupi ambayo imeendelezwa kwa kuzingatia kipengele cha mwingilianotanzu ambapo mitholojia ya kisanduku cha Pandora yenye asili ya Kiyunani imetumika. Kwa mujibu wa riwaya vijana wanapewa vifedha vidogo vidogo ili kupinga mapinduzi. Maafa mbali mbali yanayofanana na yale yaliyotoka kwenye kisanduku cha Pandora huikumba taifa wakati ambapo mambo huharibika na kukawa na vita nchini.

Hadithi ya kisanduku cha Pandora ambayo ni simulizi fupi iliyofichika katika masimulizi ya riwaya teule inapatikana katika mitholojia moja ya jadi ya Kiyunani. Katika mitholojia hii maarufu inaaminika kuwa baada ya miungu kumwumba mwanamke ilimpa jina, Pandora. Miungu hiyo ilimtunukia sifa kem kem kama urembo, ucheshi, haiba, lugha shawishi, udadisi na pia udanganyifu. Kisha mungu Zeus alimpa Pandora kisanduku kwa maagizo kwamba asikifungue. Pandora alikishikilia kwa muda mfupi lakini roho ya kudadisi ikampa hamu ya kutaka kujua kilichokuwa ndani na ikamsukuma kukifungua. Ndani ya kisanduku hicho mlitoka kila aina ya uchafu. Uchafu wa Pandora ni ishara katika riwaya inayowakilisha mateso na maovu kama vile hila, udanganyifu, vurumai, chuki na njaa. Simulizi inaendelea kueleza kuwa wakati maovu yalipokuwa yakitoka, Pandora alishtuka sana na kukifunga kisanduku ghafla, kumbe alifungia tumaini ndani! Angesubiri kidogo badala ya kufunga. Kisanduku cha Pandora pia kimetumiwa katika riwaya kama ishara ya kuwapa wanajamii hasa wanaume (kwa mujibu wa muktadha wa simulizi fupi) matumaini katika ulimwengu wa sasa wenye mateso mengi. Ni Dhahiri kuwa katika jamii ya leo mwanamume anapata madhila mengi. Hivyo, kila mwanamume anahitaji kujihami na mbinu za kukabiliana na ila zenye dhuluma zinazodumu katika bongo za wanawake. Ili kuwaelewa wanawake vizuri, ni sharti kila mwanamume aelewe vidumuvyo katika akili yake. Mintarafu ya maelezo haya taswira ya jamii ya sasa inashabihiana na kisanduku cha Pandora. Imejaa maovu na uchafu wa kila aina. Baadhi ya maovu yanayofananishwa na sanduku la Pandora, yanayorejelewa na kutajwa katika riwaya teule ni kama inavyodhihirika katika nukuu lifuatalo;

> *Coup d'etat*. Ukabila. *Ethnic Cleansing*. Wazazi wakafa, wakabakia watoto waliolazimishwa kushika bunduki. Shule wakasusia. Kwa kifupi, sanduku la Pandora lilifunguliwa upya. Lilibakia wazi maskini! **(ML. UK. 101)**

Simulizi fupi hii yenye vipengele vya kimajaribio vya uchanganyaji lugha na urejeleomatini imetumiwa kuisaidia hadhira kung'amua kwamba dhuluma imekithiri katika jamii ya kizazi cha sasa. Uovu huu unaendelezwa dhidi ya raia na viongozi wenye tamaa. Dhuluma ambayo ni hali ya kumnyima binadamu haki vile vile imebainika katika riwaya teule kwa maneno mazito yenye taashira katika usemi wa *"kunyamazisha sauti."* Mwanga zaidi unatolewa kwa maneno ya msimulizi yafuatayo;

> **Akanyamazisha sauti** za akina Marugurugu na wenzake. Mwenzake naye akamtumia ujumbe wa kuja kuangalia jinsi alivyokuwa amepiga hatua. Ujumbe wa kufuatilia kujua kama msaada wao ulikuwa wa kufaa au la. Ujumbe huu ndio ndio uliomfikishia barua iliyotokea kwao. Ilikuwa Barua ya Kumbukumbu. **(MMM. UK. 75)**

Jamii ya kisasa inadhulumiwa kwa kunyimwa uhuru wa usemi. Istilahi *"kunyamazisha"* imetumiwa kuashiria kuwa hamna uhuru. Wanajamii hawana nguvu za kuwasilisha uzalendo. Taswira inayoibuka ni kwamba viongozi wa mataifa ya Kiafrika yanayoendelea hawana nafasi ya kukosolewa. Yeyote anayethubutu kukosoa uongozi wao hunyamazishwa kwa njia tofauti tofauti. Wako wale wanaokamatwa na kuteswa ilhali wengine hufa kwa njia zisizoelezeka. Kwa mfano, barani Afrika katika nchi ya Uganda Robert Kyagulanyi Ssentamu maarufu kama Bobi Wine na Kizza Bessigye wameumizwa na utawala wa nchi kwa sababu ya kumpinga kiongozi wao kama ilivyorekodiwa katika gazeti la *East African* (tarehe 18.10.2019). Isitoshe, nchini Kenya Raila Odinga, Marehemu Charles Rubia na Marehemu Kenneth Matiba wameripotiwa kuteswa sana wakati wa utawala wa aliyekuwa rais wakati huo kama ilivyoripotiwa katika gazeti la *Daily Nation* (4.10.2013). Viongozi walafi hawawezi kuwapa nafasi wazalendo kwa hofu kuwa wataufichua ulafi na uovu wao na kuutangaza hadharani. Juhudi za uzalendo zinadidimizwa na dhuluma inaendelezwa kwa raia wasio na hatia kama ilivyodhihirika katika simulizi hii;

> "Njia nzuri ya kuhakikisha kuwa umejizika katika bongo zao ni kujitosa kwenye kiwiliwili cha utamaduni na kukwamia hapo kama ruba" ilibidi isemwe kuwa mimi ndiye yule kiongozi aliyesemwa kuwa atakuja kuikomboa jamii kutokana na pingu za maisha. Kuna ithibati ipi nyingine kuliko kule kuja na uganga wa kugeua chembe chembe? Sasa ilibidi wakumbuke uwezo wangu; nilikuwa na uwezo wa kukomboa. **(ML. UK. 12)**

Dhuluma inaendelezwa kwa kutumia ujanja. Vile vile mbinu nyingine zinazotumiwa kuwakosea haki raia kwa kuwatungia mashtaka bandia, kufanya ufisadi katika vitengo vya sheria na kuwatia watu kizuizini bila sababu.

> Ilikuwa lazima mbinu mpya zibuniwe. Mashtaka bandia. Mapatano maalum na Idara ya Sheria. Sheria mpya zikabuniwa, *Detention Without Trial*. *Preventive Detention Act.* Huu wakati wa kuijenga nchi hatuwezi kuuharibu kwa kesi zisizofaa," alisema Mzee. **(ML. UK. 12)**

Japo jamii inaogelea katika kidimbwi cha maovu mengi yaliyotapakaa kote, yapo matumaini. Ingawa mambo yameharibika nchi inaweza kupona, kuchipuka tena na kupaa kimaendeleo iwapo wenyeji watachukua majukumu yao kikamilifu. Kuna uwezekano wa kupata uhuru kutokana na madhila yaliyopo. Iwapo jamii itatia bidii kujikomboa kuna uwezekano wa kupata tumaini jipya lenye mustakabali mzuri kama inavyotajwa katika nukuu hili;

> Baadaye ilitangazwa hata kwenye redio ya taifa. Hiki ni kipindi cha mwanzo mpya. Hiki ni kipindi cha kuzaliwa upya. Ya kale hayapo tena. Mtu hawezi kuzaliwa upya asipokuwa na jina jipya na kwamba hicho kinachozaliwa upya kina uwezo mkubwa kuliko kilichokizaa **(MMM. UK. 2)**.

"Kuzaliwa upya" ni ishara ya nchi au taifa lenye mwamko mpya. Baada ya uzinduzi kutoka gizani kutakuwa na jamii mpya ambayo itapendeza zaidi kuliko jamii ya jadi. Ujenzi wa jamii

mpya utazaa kizazi kinachowajibika. Maovu ya awali kama ubadhirifu wa mali ya umma, dhuluma, vita vya kikabila, mapinduzi ya serikali, ukosefu wa ajira hasa miongoni mwa vijana, hali ya uchumi kudorora, madeni miongoni mwa mengine yatazikwa katika historia. Kizazi kipya kitang'aa gizani. Kitakuwa bora kuliko kizazi cha jadi.

## 5.0 HITIMISHO

Kwa mujibu wa riwaya, uandishi bunifu kama mwito wa kipekee huhodhi hisia na msukumo usiozuilika. Hata hivyo, imedhihirika kuwa kimuundo na kimtindo uandishi wa riwaya ya kisasa umekiuka ujadi uliozoeleka. Ukosefu wa utaratibu katika uandishi bunifu wa riwaya ya kisasa ni kioo cha jinsi jamii ya kisasa ilivyo; haina utaratibu. Taswira kamili ya jamii ya kisasa inayojidhihirisha kwa jumla ni kwamba ni jamii isiyopendelea kufuata utaratibu. Ni jamii inayofahamu mengi ambayo inayawasilisha kwa pamoja pasina kufuata mpangilio wowote; bora wayatakayo yafike kwa hadhira.

## 6.0 MAREJELEO

Barongo, Y. R. (1980). *Neocolonialism and African Politics: A Survey of the Impact of Neocolonialism on African Political Behavior*. New York: Vantage Press.

Baudrillard, J. (1988). *Selected Writings*. Stanford: Stanford University Press.

Birmingham, D. (1995). *The Decolonization of Africa.* Ohio: Ohio University Press.

Blum, L. (2004). Stereotypes And Stereotyping: A Moral Analysis *Philosophical Papers*, [online] Vol. 33. Issue 3. pp 251-289. Available at: <https://www.tandfonline.com/doi/abs/10.1080/05568640409485143> [Accessed 14 January 2020].

Bradford, S. (2007). *Diana*. London: Penguin Books.

Brown, T. (2008). *The Diana Chronicles.* New York: Anchor Books.

Jones, H. (1988). *Mutiny on the Amistad: The Saga of a Slave Revolt and its Impact on American Abolition, Law, and Diplomacy*. New York: Oxford University Press.

Junor, P. (2005). *The Firm: The Troubled Life of the House of Windsor.* London: Harper Collins Publishers.

Lunde, D.T. (1979). *Murder and Madness.* New York: Norton.

Halliwel, S. (1992). *Teaching English in the Primary Classroom.* London: Longman.

Malenya, M.M. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Fasihi Simulizi.* Mwanza: Inland Press.

Mutua, J.M., Issa, M., AbdulRahim, T. (2022). Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila. Mwanga wa Lugha 6. 15-26. Eldoret: Moi University Press.

Mutua, J.M., Issa, M. & AbdulRahim, T. (2019). Urejeleomatini katika Uwasilishaji wa Maudhui ya Dhuluma katika Riwaya ya Msichana wa Mbalamwezi (K.W.Wamitila). International Journal of Advanced Research. 7. 303-308. 10.21474/IJAR 01/9038.

Nanjira, D.D. (2010). African Foreign Policy and Diplomacy from Antiquity to the @1st Century. Santa Barbara, CA: Praeger.

Nyabunga, V.A. (2005). Uhakiki wa Bina-damu (2002) na Musaleo! (2004) na K.W. Wamitila.

Tasnifu ya Uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Osagie, I.F. (2000). The Amistad Revolt. Athens & London: University of Georgia Press.

Pakenham, T. (1992). The Scramble for Africa: Whitman's Conquest of the Dark Continent from 1876-1912. New York: Avon.

Rodney, W. (1972). How Europe Underdeveloped Africa. London: Bogle-L'Ouverture Publications.

Smith, S. B. (2007). Diana: The Life of a Troubled Princess. London: Aurum Press Ltd.

Snell, K. (2013). Diana: Her Last Love. London: Andre Deutsch Ltd.

Suret-Canale, J. (1988). Essays on African History: From The Slave Trade To Neo-Colonialism. London: Hurst.

Wacharo, J. (2013). Kanga kama Sajili Maalum ya Kisanii na Mawasiliano. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi.

Waller, R. (2014). Kenya: A History Since Independence. London: I.B. Tauris.

Wamitila, K.W. (2004). Musaleo! Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K.W. (2014). Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wilson, T. D. & Gilbert, D. T. (2003). Affective Forecasting. In M. P. Zanna (Ed.), *Advances in Experimental Social Psychology*, Vol. 35. pp. 345–411. Elsevier Academic Press. https://doi.org/10.1016/S0065-2601(03)01006-2

Yuswanto, F.A. (2015). "Diversity of Existentialism Theory, Patterns and its Reflection in Jurispundence South East Asia Journal Contemporary Business. Economics and Law.